# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA SAME

**FAHARI YA SAME**

**Maendeleo Daima**

**Toleo la Septemba,2024 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz SAME DC samedc2022**

## RC- KILIMANJARO AWATAKA WANANCHI KUJIANDIKISHA KWA WINGI DAFTARI LA MKAZI



***Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Nurdin Babu akizungumza na Wananchi wa Kata ya Chome alipofanya ziara Wilayani Same.***

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Nurdin Babu amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwenye Daftari la Mkazi ili kukidhi vigezo vya

kupiga kura kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotrarajiwa kufanyika Novemba 27 Mwaka huu.

Mheshimiwa Babu ametoa wito huo alipofanya ziara Wilayani Same ambapo alisema ili mwananchi aweze kupata haki yake ya kupiga kura ni lazima ajiandikishe kwenye Daftari la Mkazi katika zoezi la Uandikisha lililoanza Oktoba 10-11 mwaka huu.

“Tunakwenda kuchagua Wenyeviti wa Vijiji, wenyeviti wa Vitongoji na Halmashauri za Vijiji, hivyo kila mwananchi anatakiwa kujiandikisha ili atumie haki yake ya msingi ya kuchagua viongozi” alisema Mkuu wa Mkoa.

Aidha aliwataka wananchi wote wenye sifa za kugombea nafasi hizo wajitokeze kugombea ili kupata viongozi walio bora ambapo alisema kila mwananchi ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

Mheshimiwa Babu alisema baada ya kukamilika kwa zoezi la kujiandikisha wananchi waliojiandikisha wanapaswa kujitokeza kwa wingi kwenye zoezi la kupiga kura.

Akizungumza katika ziara hiyo Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni alimhakikishia Mkuu wa Mkoa kwamba wananchi wamehamasishwa na watajitokeza kwa wingi kujiandikisha na kupiga kura.

“Nikuhakikishie tu Mkuu wetu wa Mkoa kwamba Wilaya yetu tumejipanga vizuri kuhakikisha kuwa wananchi wote wenye sifa za kupiga kura wanaandikishwa kwenye daftari la Mkazi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama amesema maandalizi ya uandikishaji yamefanyika vizuri na zoezi la uandikishaji linaendele.

“Kila Kitongoji kina kituo cha kuandikisha wapigakura wa Kitongoji husika, na waandishi tayari wameshapatiwa mafunzo, hivyo uandikishaji unaendelea vizuri” alisema Bw. Mhagama

Wilaya ya Same ina Jumla ya Vijiji 100 na Vitongoji 503 ambavyo vitashiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu.

**“Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi, Jitokeze kushiriki Uchaguzi”**

## ‘HARAKATI ZA KUMKOMBOA MWANAMKE ZIMELETA TIJA’




***Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi (katikati) akifuatilia mada kwenye kongamano la Wanawake, pamoja nae ni Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni (kulia) na Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro Bi. Mercy Mollel.***

Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Bi. Mwanaidi Ali Khamisi amesema harakati mbalimbali za Kimataifa na Kitaifa zimewezesha usawa wa Jinsia kwenye ajira na kwenye nafasi za uteuzi.

Ameyasema hayo kwenye Kongamano la wanawake Wilayani Same ambapo alisema kwasasa kumekuwa na mabadiliko chanya katika ajira na nafasi za uteuzi ambapo Wanawake wamekuwa wakipewa nafasi.

Alisema Serikali imesaini mikataba mbalimbali ya Kimataifa yenye lengo la kuhakikisha Wanawake wanaingia kwa wingi kwenye nafasi za maamuzi.

Uwepo wa wagombea wa viti Maalum vya nafasi za ubunge na udiwani pamoja na kundi Maalum la wanawake kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa ni jitihada za Serikali kuongeza uwakilishi wa wanawake kwenye nafasi za maamuzi.

Akizungumza kwenye Kongamano hilo, Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni alisema Ofisi yake kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa

Halmashauri wameona umuhimu wa kuwaleta Wanawake wa Same pamoja ili waweze kubadilishana mawazo katika kukuza Uchumi.

'Lengo la kongamano hili ni kuwaleta pamoja wanawake ilikujadili fursa za kiuchumi na kuwapa elimu ya kutumia nishati Safi ya kupikia ili kutunza mazingira "alisema Mhe.Kasilda

Nae Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mheshimiwa Yusto Mapande aliwataka wanawake kutambua kuwa wao sio washindani wa wanaume.

"Naunga mkono harakati za kumkomboa mwanamke dhidi ya unyanyasaji lakini niseme kuwa wanawake sio washindani wa wanaume bali kila mmoja atimize majukumu yake"alisema Mhe.Yusto

Katika Kongamano hilo lililojumuisha wanawake zaidi ya 400 kutoka maeneo mbalimbali ya Same na nje ya Same, mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwemo Utunzaji wa Mazingira, Afya, Fursa za Uchumi, Kuzuia ukatili wa kijinsia na Elimu ya Uongozi.

## TASAF SAME YATOA MIL.436.4 RUZUKU YA UZALISHAJI



***Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Nurdin Babu(mwenye shati jeupe) akiangalia mifugo ya mnufaika Judith Kihara wa Kata ya Chome (wa pili kushoto).Mkuu wa Mkoa alifanya ziara Wilayani Same kukagua Miradi ya Maendeleo.***

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Wilaya ya Same umetoa Ruzuku ya Uwezeshaji ya shilingi Mil. 436,450,000/- kwa kaya 1,247 ili kuziwezesha kuanzisha Miradi itakayoziwezesha kuondokana na umaskini.

Akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro aliyefanya ziara kutembelea kaya hizo, Kaimu Mratibu wa TASAF Wilaya ya Same Bw. Frank Michael alisema TASAF imeanzisha Ruzuku ya Uzalishaji kwa walengwa ili kuwawezesha kuzalisha mali wenyewe ili waweze kuendesha maisha yao na familia zao.

“Walengwa waliopata Ruzuku ya Uzalishaji wanatoka Vijiji 59 kati ya Vijiji 100 vya Wilaya ya Same, Walengwa 317 hawakukidhi vigezo vya kupata Ruzuku hiyo” alisema Bw. Michael.

Alisema Ruzuku ya uzalishaji ambayo ilitolewa mwezi Mei mwaka huu imeshaanza kuonyesha matokeo chanya kwani kuna walionunua mbuzi, kuku na ndama ambao tayari wameshawanufaisha.

Akizungumza baada kumtembelea mnufaika Judith Kihara wa Kata ya Chome, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Nurdin Babu aliwataka wanufaika wa Ruzuku ya uzalishaji kuhakikisha kuwa wanaitumia vizuri ruzuku hiyo katika kuondokana na umaskini.

“Niwapongeze sana TASAF kwa kubuni Ruzuku hii na nina imani kubwa kwamba itawezesha kaya maskini kuinuka kiuchumi, lakini muendelee kuwatembelea mara kwa mara na kuwapa ushauri namna ya kuboresha wanachokifanya” alisema Mkuu wa Mkoa.

Aidha alionya baadhi ya walengwa ambao wanapokea Ruzuku ya fedha taslim kutumia fedha hizo kwa malengo tarajiwa na kamwe wasitumie kunywea pombe.

Mnufaika wa Ruzuku hiyo Bi. Judith Kihara ameishukuru Serikali kwa kuwapatia Ruzuku ya Uzalishaji ambayo aliitumia kununua mifugo ambayo inaendelea vizuri.



# WASAFIRI WANAOTUMIA BARABARA KUU YA SAME-DSM WAONYWA KUTOTUPA TAKA BARABARANI



***Afisa Afya na Usimamizi wa Taka Ngumu Wilaya ya Same, Bi. Yuster Malisa akitoa elimu ya afya kwa wananchi.***

Wasafiri wanaotumia barabara kuu ya Same-Dar Es Salaam wameonywa kuacha kutupa takataka za mabaki ya vyakula na vinywaji barabarani ili kutunza usafi wa Mji wa Same.

Onyo hilo limetolewa na Afisa Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi. Yuster Malisa wakati wa maadhimisho ya siku ya Usafi Duniani ambayo hufanyika Septemba 20 ya kila mwaka.

“Wafanya usafi kwenye barabara zetu wamekuwa wakilazimika kuokota taka zinazotupwa kutoka kwenye magari wakati Serikali ilishaelekeza magari yote ya abiria yawe na vifaa vya kutupia taka na kwa yale ya binafsi wahifadhi taka zao hadi wafike sehemu sahihi ya kuzitupa na sio kuzirusha barabarani” alisema Bi. Malisa

Alisema katika kudhibiti hali hiyo tayari hatua za kutoza faini kwa watu wanaorusha taka barabarani zimeshaanza kuchukuliwa ambapo alisema kuna baadhi ya mabasi tayari abiria wake waliorushwa taka nje wameshalipishwa faini.

Alisema lengo ni kuhakikisha Wilaya ya Same inakuwa na mazingira safi na yanayovutia ili kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Wilaya ya Same iliadhimisha siku ya usafi duniani kwenye Kata ya Hedaru kwa wananchi kusafisha maeneo ya makorongo na pembezoni mwa barabara.

Aidha aliwataka wananchi wa Same kuchangia ada ya uzoaji taka kwa wakati ili kuwezesha uzoaji taka kwa ufanisi kwenye maendeo yao.

## SAME YATEKELEZA MIRADI YA BIL 14 KWA MWAKA MMOJA



***Mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Malindi Kata ya Suji ukiwa katika hatua za umaliziaji***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imetumia Shilingi Bilioni 14 kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo kati ya fedha hizo bil 2.4 zilikuja nje ya ukomo wa bajeti.

Hayo yamebainishwa kwenye taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama kwenye Baraza la Madiwani la mwaka unaoishia Juni 30, 2024.

Katika taarifa yake iliyowasilishwa na Afisa Mipango Msaidizi Bw. Elisha Kapama ilibainisha kuwa fedha hizo zilitumika kujenga na kukarabati Miradi ya Elimu, Afya, Ujenzi wa ofisi za Kata na Vijiji na Miradi ya umwagiliaji.

Baadhi ya Miradi ya Elimu Sekondari iliyotekelezwa ni Ujenzi wa Shule mpya tatu za Sekondari za Angellah Kairuki, Malindi na Misufini Goma na mwingine ni Miradi ya Ujenzi wa nyumba tatu za walimu (2 in 1) kwenye shule za Sekondari Misufini Goma, Angella Kairuki na Malindi, miradi mingine ni umaliziaji wa mabweni kwenye shule nane za sekondari na umaliziaji wa bwalo.


"Kwa upande wa Afya Miradi iliyotekelezwa ni ujenzi wa vituo vya Afya kwenye Kata za Mtii, Ruvu na Myamba, umaliziaji na ukarabati wa zahanati nne za Masandare, Mwembe, Duma na Kankokoro, ujenzi wa nyumba ya mtumishi zahanati ya Myamba na ununuzi wa vifaa tiba kwenye zahanati tano za Kirongwe, kalung'oyo, Kidunda, Kankokoro na Mgando pamoja na vituo vya Afya vitano vya Myamba, Mtii, Hedaru, Ruvu na Kisiwani' alisema

Kwa upande wa elimu Msingi Miradi iliyotekelezwa ni Ujenzi wa madarasa mapya zaidi ya 40, matundu ya vyoo 114 na ununuzi wa madawati 1,295 na ujenzi wa nyumba nne za walimu pamoja na ukarabati wa nyumba mbili za walimu.

Akizungumza kwenye kikao hicho Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mheshimiwa Yusto Mapande ameshauri Halmashauri kuhakikisha kuwa Miradi viporo inapewa kipaumbele cha umaliziaji wakati Serikali inapoanza mwaka mpya wa fedha 2024/2025.



# KATA TATU ZAPATIWA PIKIPIKI



***Kutoka kushoto ni Diwani wa Kata ya Chome Mheshimiwa Heriel Boniface anayefuatia ni Diwani wa Kata ya Vudee Mhe Yoeza Mnzava na Diwani wa Kata ya Myamba Mhe. Gayson Kiondo wakifurahia baada ya Kata zao kukabidhiwa pikipiki.***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imekabidhi pikipiki tatu kwa watendaji wa Kata za Myamba, Vudee na Chome ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao.

Akikabidhi pikipiki hizo zilizotolewa na Ofisi ya Rais Tamisemi, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mheshimiwa Yusto Mapande aliwaagiza watendaji waliopatiwa pikipiki kuhakikisha kwamba wanazitunza pikipiki hizo.

"Hizi pikipiki ni mali ya Serikali hivyo hakikisheni mnazitunza ili zidumu na kuendelea kufanikisha majukumu ya kazi, zisitumike vinginevyo"alionya Mapande.

Akitoa shukrani kwa kupatiwa pikipiki Diwani wa Kata ya Myamba, Mheshimiwa Grayson Kiondo aliishukuru Serikali kwa msaada huo na kuahidi kusimamia utunzaji wa pikipiki hiyo.

"Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu kwa kutupatia pikipiki, ninachoweza kuahidi ni kuongeza tija kwenye utendaji ikiwa ni pamoja na kuongeza ukusanyaji wa mapato"alisema Diwani huyo.

# KAMATI YA FEDHA YAPONGEZA USIMAMIZI MZURI WA UJENZI WA MABWENI



***Bweni la Shule ya Sekondari Kibacha likiwa kwenye hatua ya umaliziaji***

Kamati ya fedha, Uongozi na Mipango ya Halmashauri ya Wilaya ya Same imetembelea na kukagua Miradi ya Ujenzi wa mabweni matatu kwenye Shule za Sekondari za Kibacha na Makanya ambapo ilieleza kuridhishwa na maendeleo ya ujenzi.

Katika ziara hiyo iliyoongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Emanuel Mhina alieleza kuridhishwa na Maendeleo ya Ujenzi wa mabweni hayo ambayo yapo kwenye hatua ya umaliziaji.

Akizungumza baada ya kutembelea mabweni mawili yanayojengwa kwenye Shule ya Sekondari Kibacha, mjumbe wa Kamati hiyo Mheshimiwa Mathias Mrita ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Same aliwapongeza walimu kwa usimamizi nzuri wa Ujenzi huo.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Mhina alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Wilaya ya Same fedha za kuwezesha Miradi hiyo.

Akitoa taarifa ya Ujenzi wa mabweni mawili kwenye Shule ya Sekondari Kibacha, Katibu wa Kamati ya Ujenzi Mwl.Daudi Makorenda alisema katika bweni la kwanza walipokea mili.80 toka mpango wa EP4R na baadae wakaongezewa mil.20 toka mapato ya ndani ya Halmashauri.

Alisema kwa bweni la pili wamepokea Shilingi mil.100.9 Fedha ambazo zimetumika kujenga bweni la pili na kumalizia Ujenzi wa bweni la kwanza ambapo alisema

mabweni yote mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 160 yanatarajia kukamilika mapema mwezi Septemba,2024.

Akitoa taarifa ya Ujenzi wa bweni la wavulana kwenye Shule ya Sekondari Makanya,Mkuu wa Shule hiyo Mwl.Bernad Mgaya alisema awali Shule hiyo ilipatiwa mil.80 kwaajili ya Ujenzi wa bweni lakini hazikutosha hivyo wameongezewa mil.80.5 toka Serikali kuu na ndizo zinazotumika kukamilisha bweni hilo.

## MAAFISA KILIMO SAME WAPATIWA VISHKWAMBI

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imewapatia Maafisa Kilimo wa Wilayani Same vishikwambi 39 ili kuwezesha taarifa mbalimbali za kilimo kutolewa kwa wakati kwa njia ya mtandao na kuwezesha maafisa kilimo kuingia kwenye mifumo mbalimbali kwaajili ya kutoa na kupokea taarifa zitakazowezesha uboreshaji wa kilimo.

Akikabidhi vishkwambi hivyo ,Kaimu Afisa Tawala Wilaya ya Same Bw. Sixbert Sarmett alisema sekta ya kilimo ni kubwa na imebeba hatma ya watanzania hivyo amewataka maafisa kilimo kuhakikisha kuwa wanatumia zana hizo vizuri ili kuboresha kilimo.

"Leo tumewakabidhi vitendea kazi,tunatambua shughuli nyingi za serikali zinatumia mifumo hivyo mkavitumie vyema vishkwambi hivi kutatua changamoito za kilimo na kuvitunza viweze kudumu "Alisema Bw. Sarmett

Afisa Kilimo Dkt. Cainan Kiswaga alisema kuna jumla ya vishikwambi 39 ambavyo vimeletwa kwa ajili ya maafisa Kilimo wote katika kata zote ambavyo vitatumika katika kuhifadhi taarifa mbalimbali zinazohusu sekta hii ya kilimo.

"Tunaamini kuwa maafisa kilimo wote waliopata vishikwambi hivi itawawia rahisi kutekeleza majukumu yao hasa ya ukusanyaji na utoaji wa taarifa sahihi kwa wakati" alisema Dkt.Cainan



# NEEMA KWA WAKULIMA WA KAHAWA



***Mshauri  wa Kilimo wa Wilaya ya Same Bw.Fidel Bigula akionyesha mbegu mpya ya Kahawa aina ya Arabica Compactss***

Wakulima wa Kahawa Wilayani Same wameshauriwa kubadilika kutoka kutumia mbegu za zamani ambazo zinachelewa kukomaa na kuanza kutumia mbegu zilizoboreshwa za Arabica Compact ambazo zinakomaa mapema.


Akizungumza kwenye maonesho ya Nane nane Kanda ya Kaskazini Mshauri wa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Fidel Bigula amesema mbegu ya Arabica Compact ni mbegu mpya ambayo inazaa ndani ya miaka mitatu tangu ioteshwe na inazaa sana kuliko mbegu za zamani.

“Mbegu hii imeboreshwa na watafiti kutoka Kituo cha Utafiti wa Kahawa TACRI ambapo tangu imeanza kusambazwa imeonyesha mafanikio kwa wakulima kwani inakomaa mapema na haishambuliwi na wadudu” alisema

Alisema kwa Wilaya ya Same tayari mbegu hiyo imesambazwa katika Kata mbalimbali na inaendelea kusambazwa ili kuhakikisha wakulima wote wanaachana na mbegu za zamani ambazo zina gharama kubwa ya kuzihudumia na uzao wake ni mdogo.

Bw.Bigula alisema mbegu ya Arabica Compact hutoa hadi kilo tano katika mchumo mmoja tu  kwenye shina moja wakati ukilinganisha na  mchumo mmoja wa mbegu za asili haufiki hata kilo tatu.

# JINSI NG'OMBE ANAVYOWEZA KUONDOA UMASKINI



***Ngombe waliohamilishwa ambao wana uwezo wa kuzalisha maziwa Zaidi ya lita 25 kwa mkamuo mmoja.***

Ng'ombe ni mnyama ambaye watu wengi wamezoea kumfuga kwaajili ya kupata maziwa ya familia na wengine kwa matumizi ya kulima mashamba lakini ng'ombe akitunzwa vizuri anaweza kuondoa umaskini kwenye jamii.

Mshauri wa Mifugo Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Zawadi Msambaa anasema kupitia njia ya uhamilishaji mifugo Wilaya imefanikiwa kuzalisha ng'ombe mwenye uwezo wa kutoa lita 30 za maziwa kwa mkamuo mmoja tu.

Akizungumza kwenye Banda la Mifugo la Halmashauri ya Wilaya ya Same kwenye maonesho ya nanenane alisema Wilaya imepeleka ng'ombe hao kwenye maonesho ya nanena ili wafugaji wengine waweze kujifunza ufugaji ulio bora.

"Umefika wakati kwa wafugaji kuachana na ufugaji wa kizamani wafuge ufugaji wa kisasa ambao unaweza kuleta tija kwenye maisha yao ambao ni ufugaji wa kibiashara" alisema

Bw.Zawadi alisema Wilaya imekuja na teknolojia nyingi kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji kufuga kisasa ambapo wafugaji wanapatiwa huduma ya uhamilishaji wa ng'ombe wa maziwa kupitia program ya mbegu za ruzuku kutoka Serikali kuu.

"Ufugaji wa kisasa unapunguza migogoro ya ardhi kwani mfugaji ana uwezo wa kufuga mifugo michache na ikamuwezesha kujimudu kimaisha" alisema

Mfugaji wa Ng'ombe hao kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Lameck Mbise alisema ng'ombe anaowafuga wote wana uwezo wa kuzalisha maziwa lita 25 hadi 30 kwa mkamuo mmoja" alisema

Bw.Lameck ameishukuru Serikali kwa kufanyia mifugo yake uhamilishaji hivyo kuweza kuzalisha ng'ombe walio bora ambao wanamsaidia kukidhi mahitaji ya familia.

"Ng'ombe wana wana faida kubwa kama kupata maziwa, mbolea na ngozi" alisema na kuongeza kuwa ufugsji wa ng'ombe umemsaidia kuongeza pato la familia na kuweza kuhudumia vyema familia.

Mshauri wa Mifugo Wilaya ya Same

Bw.Msambaa amesema kwa mfugaji yeyote anayehitaji huduma ya uhamilishaji awasiliane na Afisa Mifugo aliye kwenye Kata yake au afike Ofisi za Halmashauri kwa Msaada Zaidi.

## DC KASILDA APONGEZA SHULE ZILIZOFANYA VIZURI



***Mkuu wa WIlaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni akizungumza na Waalimu.***

Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni ,amewapongeza wadau wa elimu kutoka shule mbalimbali zinazomilikiwa na serikali,watu binafsi na mashirika ya dini zilizofanya vizuri kwenye matokeo ya mitihani ya Taifa mwaka jana.

Mhe. Kasilda ameeleza kufurahishwa na uboreshaji wa elimu kwenye shule hizo ambazo zimefanya vizuri, pia amesema serikali itaendelea kutoa ushirikiano ili shule hizo ziendelee kufanya vizuri zaidi.

" Serikali tutaendelea kutoa ushirikiano ili muweze kufanya vizuri zaidi kwenye elimu,lakini pamoja na pongezi hizi ninaomba sana zile changamoto ambazo zinasababisha wanafunzi kutofanya vizuri mkazifanyie kazi kwani lengo kuu la kikao hichi cha elimu ni kuhakikisha ufaulu unaongezeka"alisema

Shule za Sekondari za binafsi zilizofanya vizuri matokeo ya kidato cha nne mwaka 2023 ni Shule za wasichana Joyland, St.Clara na Kandoto pamoja na shule ya Wavulana St.Joachim ambapo kwa shule za Serikali zilizofanya vizuri ni Chalao,Kirangare,Bangalala na Bombo.s

Afisa Elimu Msingi Wilaya ya Same Mwl.Marclaud Mero alisema wilaya ya Same ina jumla ya shule za Msingi za Serikali 188 na za binafsi 18 hivyo kufanya jumla ya shule za msingi 206, shule za Sekondari zipo 66 kati ya hizo 46 ni za Serikali na 20 ni za sekta binafsi na chuo cha Ualimu kimoja ambacho kipo chini ya dini.

"Kikao hiki cha wadau wa elimu ni cha muhimu katika kutathimini maendeleo ya elimu na kutathimini matokeo ya mitihani iliyopita hivyo mnapaswa kushiriki kikamilifu katika kuandaa mikakati ambayo itasaidia kuinua taaluma na ufaulu katika Halmashauri yetu" alisema Mwl.Mero.

Kwa upande wake Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Same Bw. Godfrey Sebulu amesema "kwa mujibu wa kanuni ya 12 ya Utumishi wa walimu ya mwaka 2016 inawatambua wakuu wa shule ndio wenye mamlaka kamili ya usimamizi wa maadili ngazi ya shule hivyo wanapaswa kuwasimamia kikamilifu walimu walio chini yao"

Mthibiti Ubora wa Elimu Wilaya ya Same Bw.Calist Youze alisema suala la ufaulu wa wanafunzi linahusisha Serikali, walimu ,wanafunzi na wazazi,hivyo kila mmoja anapaswa kusimama kwenye nafasi yake.

Hata hivyo kikao hicho kiliazimia kuwasuala la nidhamu na maadili ya mwanafunzi yaanzie kwa wazazi,kuwe na ushirikiano mzuri katika swala taaluma kati ya walimu na wazazi, walimu watumie mbinu mbalimbali kuwajengea wanafunzi mazoea ya kujisomea, kila siku wanafunzi wapewe maswali ya Hesabu ili kuongeza ufaulu kwenye somo la Hisabati.

# WANAFUNZI 6,151 WAHITIMU DARASA LA SABA SAME



Jumla ya wanafunzi 6,151 wamefanya mitihani ya kuhitimu darasa la Saba mwaka 2024 Wilayani Same ambapo kati yao wanafunzi 3012 ni wavulana na wasichana ni 3139, takwimu hizo zinajumuisha wanafunzi wenye uoni hafifu ambao ni 5 kati yao wavulana ni 4 na Msichana ni 1.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama amesema Wilaya ina matarajio makubwa ya ufaulu kwa wanafunzi hao kwani maandalizi yalifanyika vizuri.

Halmashauri ya Wilaya ya Same ina jumla ya Shule za Msingi 206 ambapo shule 188 ni za Serikali na 18 ni za binafsi, ambapo shule zenye watahiniwa wa Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi ni 196 .

Afisa Elimu Awali na  Msingi  wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Marclaud Mero alisema shule hizo 186 ni za Mfumo wa Kiswahili na 10 ni za Mfumo wa Kiingereza (English Medium Schools) zinazomilikiwa na Taasisi Binafsi.

Bw. Mero alisema wanafunzi waliofanya mtihani wa Taifa mwaka huu waliandikishwa darasa la kwanza mwaka 2018 wakiwa wanafunzi 6243 ambapo kati yao wavulana walikuwa 3066 na wasichana ni 3177.

“Idadi ya wanaomaliza imepungua kidogo kutokana na baadhi ya wanafunzi kuhama Wilaya” alisema




***Wadau wa Maendeleo Wilaya ya Same walipokutana kuandaa vipaumbele vya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025-2050 ambapo wadau hao walitaja vipaumbele vyao kuwa ni kuweka mazingira ya kushawishi uwekezaji wa Viwanda vikubwa, kipaumbele kingine ni kuwa na vyuo vikuu pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa maji ya uhakikika kwa kila mwananchi.***



***Muuguzi wa Hospitali ya Mji –Same Mary Mavura akiwaelekeza kina mama namna sahihi ya kumnyonyesha mtoto katika maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji maziwa ya mama Duniani.Wiki ya Unyonyeshaji huadhimishwa Agosti 1-7 kila mwaka.***



***Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mhe.Emmanuel Mmasa na Mkurugenzi wa Halmashauri Bw.Jimson Mhagama wakifurahia ubora wa kinawia mkono cha Jamii(Public hand washing point) kilichojengwa kwenye zahanati ya Makanya Kitivo wakati Kamati ya Fedha ilipofanya ziara kwenye Zahanati hiyo.***



***Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama akifafanua jambo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani,Kulia ni Mwenyekiti wa Hamashauri Mhe.Yusto Mapande na Kushoto ni Afisa Serikali za Mitaa Mkoa Bw.Jasper Ijiko.***



***Masanduku ya kura yakiwa tayari kwaajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Novemba 27 2024***



***Mshindi wa Mchezo wa draft kwenye Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Watumishi wa Serikali za Mitaa(SHIMISEMITA)yaliyofanyika Jijini Mwanza Bi. Anne Mkwizu ( kulia) akikabidhi kikombe cha ushindi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama ,kushoto ni Afisa Michezo na Utamaduni wa Wilaya ya Same Bw.Nevlin Nyange.***



***Mwenyekiti wa Wakulima wa Tangawizi Mamba Myamba Bw. Mbaraka Ally (kulia) akiwauzia wateja Tangawizi kwenye banda la Halmashauri ya Wilaya ya Same kwenye Maonesho ya Nanenane Kanda ya Kaskazini yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Themi, Njiro mkoani Arusha.***

UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA
JIANDIKISHE PIGA KURA
2024
OFISI YA RAIS TAMISEMI



**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**S.L.P 138, SAME**

**Mhariri wa Mkuu: Jimson Mhagama**

**Mhariri wa Habari: Amina Sangawe**

***Septemba, 2024 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz SAME DC samedc2022***